

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Ruvuma:

SIMU NA. 025 – 2602256

025 - 2602238

Email: das.tunduru@ruvuma.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Tunduru,  
2 Barabara ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,  
S.L.P. 6,  
57681 TUNDURU, RUVUMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.BA.105/458/01/C/113

01/10/2024

KWA WANANCHI WOTE,  
WILAYA YA TUNDURU.

**YAH: TANGAZO LA VIJANA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA  
UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI) MWAKA 2024/2025**

Rejea mada tajwa hapo juu.

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Tunduru anawatangazia Wananchi wote Tunduru wenye nia na sifa ya Kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa kujitolea kwa (Hiari) mwaka 2024/2025 waombe nafasi hizo. Aidha , maombi yote yatumwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Wilaya Tunduru S.L.P. 06 Tunduru, baada ya kupitishwa na Mtendaji wa Kijiji/Kata unachoishi. Barua zisipitishwe Posta, ziende kwa mkono Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Tunduru.

Mnakumbushwa kuwa, mwisho wa kuleta maombi Ofisini kwa Mkuu wa Wilaya ni Jumapili tarehe 06/10/2024 Saa 6:00 Mchana (Ofisi itakuwa inaendelea kupokea maombi siku ya Jumamosi na Jumapili kwa tarehe tajwa), na Usaili utafanyika siku ya Jumanne tarehe 08/10/2024 Saa 2:30 Asubuhi.

**Sifa za Mwombaji** ni kama zilizoorodheshwa hapo chini:-

1. Awe raia wa Tanzania
2. Umri:
  - a) Kwa vijana wenye elimu ya Darasa la Saba umri kuanzia miaka 16 hadi 18, aliyemaliza elimu ya msingi kuanzia mwaka 2021, 2022 na 2023 awe na cheti cha kumaliza elimu msingi.

- b) Vijana wenye Elimu ya kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka 20, aliyemaliza elimu ya sekondari kuanzia mwaka 2021, 2022 na 2023 awe na cheti halisi cha kumaliza elimu ya sekondari (Secondary Leaving certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic certificate). Awe na ufaulu wa Daraja la kwanza hadi Daraja la nne. Kijana Mwenye Daraja la Nne awe na ufaulu wa alama kuanzia 26 hadi 32.
  - c) Vijana wenye Elimu Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka 22, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia mwaka 2021, 2022, 2023 na wawe na vyeti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu kuanzia Daraja la kwanza hadi Daraja la Nne.
  - d) Vijana wenye elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka 25. Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
  - e) Vijana wenye elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26, awe na vyeti vya Sekondari na Cheti cha Chuo.
  - f) Vijana wenye elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 27, awe na vyeti vya Sekondari na Cheti cha Chuo.
3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).
  4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
  5. Awe na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).
  6. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate)

7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalumu cha kuzuia magendo wala kuajiriwa na Idara nyingine ya Serikalini.
8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa kundi la kujitolea na kundi la lazima (Mujibu wa sheria).
9. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
10. Angalizo: Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kazi za kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

**Mwisho:** Zingatia muda wa kutuma maombi na masaa ili pia usitoe *Rushwa* ya aina yoyote na mahali popote.



Milongo Sanga  
**KATIBU TAWALA WILAYA  
TUNDURU.**

**Nakala:** Mkuu wa Wilaya,  
**TUNDURU** - (Aione kwenye jalada)

Maafisa Tarafa wote,  
**TUNDURU.**

Maafisa Watendaji Kata na Watendaji wa Vijiji wote,  
**TUNDURU.**

Mbao za Matangazo zote,  
**TUNDURU.**